




PreK 4 ME, Uhusiano wa Familia
SOMO LA 4: RANGI MBALIMBALI

Muhtasari wa Somo la 4: Rangi Mbalimbali


Tutaanza kugundua rangi mbalimbali ulimwenguni, tukiwa darasani. Tutajifunza kuhusu kazi za rangi duni-ani na katika mazingira. Wanafunzi watajaribu kuchanganya rangi, ikiwemo mipunguzo na mishiko, tunaimarisha msamiati wetu zaidi. Katika upande wa uigizaji, wanafunzi watashuhudia uoshaji na ukaushaji katika sehemu ya kufulia nguo. Tunazidi kuimarisha stadi zetu za hisabati kupitia michezo ya hisabati inayohusu kuhesabu mbele na nyuma, kulinganisha na kujifunza kupokezana zamu na kushiriki.

VITABU VYA SPOTLIGHT VYA SOMO LA 4




Max's Dragon Shirt

Cha: Rosemary Wells




Dog's Colorful Day

Cha: Emma Dodd



The Color of Us

Cha: Karen Katz



The Lion and the Little Red Bird

Cha: Elisa Kleven

Picha zimepakuliwa katika amazon.com

Vitabu vingine vya mwezi huu ni pamoja na...

Is It red? Is It Yellow? Is It Blue?
cha Tana Hoban

Perfect Square cha Michael Hall

Sugaring cha Jesse Haas

Backyard Birds cha Robert Bateman

Nyimbo, Herufi na Michezo ya Lugha

Wanafunzi darasani wanapenda mazoezi yaliyo katika wimbo huu! Soma pamoja na mtoto wako na umwombe akufunze vitendo hivi huku akivitaja

SIMAMA

Simama, Zunguka.

Piga makofi mara nne; Usiketi.

Piga makofi tena; Inama.

Pigisha mguu chini; Acha sasa

Punga mkono wako; Kunja magoti mawili.

Keti chini tena, na unitazame.



Muundo wa picha Image form Pixabay

Angalia sehemu inayofuata uone mazoezi ya nyumbani



Wezesha masomo ya nyumbani kupitia mazoezi haya ya ziada

Sayansi, Mbinu za Kujifunza, Sanaa na Stadi za Kusogeza Misuli

Ziara ya Rangi

Kwa kurejelea ukurasa huu, mpeleke mtoto wako katika Ziara ya Rangi. Unaweza kumpeleka nje, nyumbani, kwenye maktaba, dukani—popote pale!

Mwambie achore picha, au aonyeshe, visanduku kwa vitu anavyoona vinavyolingana na kalamu za rangi katika kila kisanduku.

Zungumzia rangi, vifaa na vitu vingine vina vyofanana na rangi hizo!

Sayansi, Afya, Kusogeza Misuli, Mbinu za Kujifunza

Kula Upinde-Mvua

Hii ni njia ya kufurahisha ya kujumuisha rangi wakati wa kula vitafunio! Tumia vitafunio nyumbani, au upange safari kwenda kwenye duka la vyakula kununua bidhaa mpya. Chagua vyakula 3 au 4 vyenye rangi mbalimbali na muviandae pamoja na mtoto wako. Pilipili ya rangi, tufa, biskuti, jibini—vyakula huwa na rangi mbalimbali!

Hisabati, Hisia-jamii, Mbinu za Kujifunza, Lugha na Masomo ya Jamii

Siku ya Kufua

Ni siku ya kufua! Mwambie mtoto wako akusaidie kupanga nguo kulingana na rangi. Unaweza kumwambia azipange katika njia mbalimbali, ikiwemo:

- ◇ Nguo zenye rangi hafifu na nzito
- ◇ Rangi nyeusi, nyeupe na nyekundu
 - ◇ Soksi zinazofanana

Zungumzia rangi, mishiko mbalimbali unayoona, jinsi unavyohisi ukigusa vitambaa.



Picha kutoka Pixabay

Ujumbe kwa wazazi na familia: Kufanya jambo mara kwa mara ni Muhimu

Wanafunzi hustawi kwa kufanya jambo mara kwa mara: katika shughuli zao za kila siku, somo, na hata vyakula wanavyopenda!

Kadri unavyofanya mambo mara kwa mara, ndivyo watoto wako watakavyofurahia. Wanapojua watakachotarajia, wataishi wakiwa na amani. Ikiwa umebadilisha ratiba yako, wafahamishe mapema ili waweze kujiandaa.

Hatua hii ni muhimu haswa katika matarajio ya tabia na nidhamu. Watoto wanapaswa kufahamu vyema wanachoruhusiwa na wasichoruhusiwa kufanya. Wanapaswa pia kufahamu adhabu watakapata kwa kukiuka kanuni.

Kwenda katika Ziara ya **RANGI**

Tembea nje na utazame vitu vyote vinavyokuzingira. Tafuta vitu unavyoona viwakilishe kila rangi. Chora picha ya kila kipengee unachopata katika kisanduku kinachofanana cha rangi.

